


**HATUA ZA KUZINGATIA  
UNAPOTATHMINI ATHARI  
ZA ULINZI WA DATA KATIKA  
MASHIRIKA MADOGO**



**Strathmore University**

*Centre for Intellectual Property and  
Information Technology Law*

Mwakani 2019, Kenya ilipitisha Sheria ya Ulinzi wa Data (Data Protection Act, 2019 au DPA ). Sheria hii inaelekeza kuwa kabla ya shughuli za usindikaji wa data binafsi, kufanywe tathmini ya athari za usindikaji huo kwa haki za wenye data. Tathmini hii inajulikana kama Data Protection Impact Assessment(DPIA)

Kwa vile kuna kampuni na mashirika mengi yaliyo kuwa yamekusanya na kutumia data za watu katika shughuli zao, mashirika haya yanahimizwa kufanya DPIA ili kutambua athari za data walizonazo.

## Je, ni nani wanahusika katika shughuli za usindikaji wa data?

### Mwenye Data Husika

Huyu ni yule mtu amabaye data inahusu. Katika shirika, data subjects waweza kuwa wateja wako, wafanyikazi, jamaa za wafanyikazi wako, wasambazaji wa bidhaa, washirika wenzako, na makandarasi.

### Mtawala wa Data

Ni yule anayeamua jinsi data itatumika na mbinu za kuendeleza michakato ya usindikaji wa data hiyo. Katika mashirika mengi, data controller aweza kuwa bodi la shirika, ama mweye biashara.

### Msindikaji wa Data

Ni mtu yeyote anayesindika data. Kwa mfano, shirika linaweza kuwa na mfumo wa kulipa wafanyikazi ambao unamilikiwa na shirika lingine.

## Je, usindikaji data unajumuisha nini?

Sheria ya Ulinzi wa Data inafafanua kuwa usindikaji unajumuisha vitendo vifuatavyo:

- ukusanyaji, kuweka rekodi, kupanga data;
- kuhifadhi, kubadilisha data;
- kupata na kutumia data;
- kutoa taarifa au kusambaza habari; au
- kuleta pamoja, kuweka vizuizi, kufuta au kuharibu data

Mifano ya usindikaji wa data katika mashirika madogo ni kama:

- kusindika mishahara ya wafanyakazi
- kuchambua wateja ili kujifunza kitu kuhusu tabia za matumizi yao
- kutuma ujumbe kwa wateja
- kuchukua maelezo ya wateja ambao kuhudhuria vipindi vya mafunzo
- kuharibu faili za zamani zenye maelezo ya wateja zisizohitajika
- kuhifadhi faili za zamani zinazohitajika

# Ni hatua gani shirika linaweza kuchukua ili kufanya DPIA?

Kuna njia mbalimbali za kufanya DPIA. Mwongozo huu unatoa hatua sita za DPIA ambazo zaweza kusaidia mashirika madogo kutathmini athari za data walizo nazo na pia kupunguza athari hizo.

## Hatua ya Kwanza

### Maelezo kuhusu shughuli za usindikaji wa data

---

Baadhi ya mambo mengine unyohitaji kufanya katika hatua hii ni:

- Orodhesha data zote unazosindika
- Pia, tambulisha na utoe maelezo kuhusu data unayosindika. Mifano ya data ni kama maelezo ya wafanyakazi wako, watu walioshiriki katika semina zako, au maelezo ya wateja/wanunizi katika duka lako, mbinu walizotumia kulipa, na kadhalika;
- Kwa kila data, orodhesha sababu zote za kuhitaji data hiyo;
- Kwa kila shughuli ya usindikaji, toa maelezo kuhusu jinsi usindikaji huo unaendelezwa; kwa mfano jinsi data inakusanywa, inavyosambazwa, inavyobadilishwa na inavyohifadhiwa.
- Pia orodhesha mahali na maeneo yote halisi usindikaji wa data unaendelezwa.

- Toa maelezo ya wakati shughuli za usindikaji wa data zinafanyika, kwa mfano, kama zinafanywa kila mwezi au kila mwaka. Mwishowe, orodhesha watu wote na kampuni zote zinazohusika katika usindikaji wa data iliyokusanywa.

Maelezo kuhusu shughuli za usindikaji wa data yatasaidia shirika lako kufahamu shughuli zote za usindikaji zinazotekeleza, na pia kumuelezea mwenye data husika sababu za kukusanya data yake. Isitoshe, ni muhimu pia kuunda miundo ya kuwajibikaji ili kuweza kujua wanaosimamia sehemu mbalimbali za shughuli hizo za usindikaji.

---

Katika hatua hii, unaweza kutumia mbinu kadhaa kuchambua usindikaji wa data katika shirika lako. Baadhi ya chambuzi hizi ni:

- 1. Uchambuzi wa kanuni** – Sheria ya Ulinzi wa Data (Data Protection Act, 2019) imeorodhesha kanuni nane za ulinzi wa data zinazopaswa kufuatwa wakati wa usindikaji. Msindikaji anapaswa:
  - i. kuzingatia faragha/usiri wa wenye data;
  - ii. kutekeleza usindikaji kwa njia ya haki na iliyo halali;
  - iii. kuwa na kusudi maalum na lengo mwafaka ya kuendeleza usindikaji huo;
  - iv. kukusanya data toshelevu;
  - v. kumpa mteja wako maelezo ya kibusara kuhusu sababu za kuchukua data fulani;
  - vi. kuweka data sahihi;
  - vii. kuhifadhi data kwa muda unaohitajika; na
  - viii. kuhakikisha kuwa data inayosindikwa nje ya Kenya inasindikwa katika nchi zilizo na sheria mwafaka za ulinzi wa data.
- 2. Sababu/Masilahi Mwafaka** - Shirika lolote linalosindika data linapaswa kuwa na sababu halali za kusindika data husika. Ikiwa halina sababu halali, usindikaji unapaswa kusimamishwa, na data hiyo kutupiliwa mbali, ili kuzuia matumizi mabaya na haramu ya data hiyo. Mfano wa sababu mwafaka ni shirika kukusanya data ya watu waliohudhuria sherehe yao ili kuwajibika kifedha; au shirika kukusanya nambari za simu na maelezo mengine ya kuwasiliana na wateja ili kuwasiliana nao badaye.

Ili kupima na kutambulisha sababu mwafaka, unaweza uliza haya maswali;

  - a) Shughuli zako za usindikaji wa data ni zipi?
  - b) Je, kwa nini unaokota na kusindika data binafsi? Ni kwa mujibu wa sheria?
  - c) Unakusanya data ya aina gani ili kuendeleza shughuli za usindikaji?
  - d) Data itahifadhiwa kwa muda gani?
  - e) Ni aina gani ya data haihitajiki?
  - f) Unahakikishaje kuwa data iliyokusanywa ni bora?
  - g) Kwa kila shughuli ya usindikaji wa data, ni kwa nini unakusanya data unayokusanya? Kwa mfano ni kwa ajili ya kufuata sheria fulani, au ni kwa ajili ya kuweka vitabu vya kifedha (accounting)?
- 3. Ulazima na Usawa** - Lazima michakato ya usindikaji wa data yalingane na sababu mwafaka za kutekeleza usindikaji huo. Zaidi ya hayo, njia za kufikia matokeo ya usindikaji yanafaa kuwa yenye ubora wa hali ya juu, yakilinganishwa na njia zingine,

ili kulinda haki za wateja wako. Ni muhimu kukumbuka kuwa, ijapo kuwa una sababu na masilahi yako mwafaka, lazima masilahi na sababu hizo zisawazishwe na haki na masilahi ya wateja wako.

Ili kuchunguza na kuchambua kama shughuli za usindikaji ni za lazima na zenye usawa, uliza maswali haya:

- a. Ni data gani inahitajika ili kufanikisha sababu mwafaka?
- b. Ni haki zipi za mteja zinaweza athiriwa na data unayokusanya?
- c. Je, data uliyo nayo ikawekwa wazi, ni watu wangapi wanaweza athiriwa?
- d. Unalindaje faragha ya wateja wako na ya kila mtu aliyena uhusiano na data hiyo?

Baada ya uchambuzi huu, hatua unazoweza kuchukua ili kupunguza athari kwa wenye data ni kama;

- a. Kusimamisha ukusanyaji wa data zisizohitajika.
- b. Kuunda mpango wa kustaafuau kufuta data zisizohitajika.
- c. Kuunda taratibu za aarifa ili kuwasiliana na wateja husika kuhusu matukio wanayopaswa kujua kuhusu data zao
- d. Kuunda taratibu zinazo waruhusu wenye data husika kuchagua michakato za usindikaji wasizotaka kushiriki.
- e. Kuunda kamati za kusimamia shughuli za usindikaji mara kwa mara, kwa mfano, kamati za ulinzi wa data

**4. Uchambuzi wa Wasifu/Profaili** – Kulingana na DPA, uchambuzi wa wasifu (profiling) ni matumizi ya usindikajiwa moja kwa moja kwa mashine kuchambua au kutabiri sifa za mtu kwa kutumia ujuzi wa maelezo yake ya kibinafsi; kama vile maelezo kuhusu kabila, utamaduni, umri, na kadhalika. DPA inalinda wateja wako dhidi ya maamuzi ya moja kwa moja ya mashine. Nyakati unazoruhusiwa kutumia uamuzi wa moja kwa moja ya mashine ni;

- Ikiwa uamuzi huo unahitajika ili kutimiza malengo ya mkataba (contract);
- Ikiwa kuna sheria inayolinda maslahi ya wateja wako; ama
- Pale ambapo mteja wako amekubali matumizi ya uamuzi wa moja kwa moja kupitia mashine

Unapoendeleza uchambuzi wa wasifu, unafaa kuwaeleza wenye data kuhusu data itakayosindikwa, unavyozingatia michakato hiyo ya kiotomatiki, na mipango iliyoko ilikutathmini athari za usindikaji wa kiotomatiki.

Maswali ya kuuliza unapofanya uchambuzi wa wasifu ni;

- Ni shughuli gani za usindikaji wa data zinazotumia usindikaji otomatiki?
- Ni maamuzi gani katika usindikaji yanafikiwa kwa njia ya kiotomatiki pekee?
- Je, wateja wanajua uamuzi wa kiotomatiki hutumiwa?
- Je, wateja wako wanaweza kata rufaa ikiwa hawajaridhika na maamuzi ya kiotomatiki?

Baada ya kukamilisha uchambuzi wa wasifu, unaweza chukua hatua zifuatazo:

- Tengeneza taratibu za kuhusisha binadamu kwenye maamuzi ya kiotomatiki
- Unda taratibu zinazoruhusu wateja kupinga maamuzi ya kiotomatiki
- Unda njia za mawasiliano ili kuwajulisha wateja kuhusu maamuzi ya kiotomatiki na njia zinazopatikana za kupinga maamuzi hayo.

**5. Uchunguzi wa Faragha Bunifu na Faragha Chaguo-msingi**– Faragha yapaswa kuzingatiwa katika ujenzi, usimamizi na utendaji wowote wa mifumo ya usindikaji wa data. Faragha bunifu inasisitiza kuhusishwa kwa faragha wakati wa ukuzaji wa mifumo. Nayo faragha chaguo-msingi inamaana kuwa baada ya mifumo kuwekwa, faragha ya hali ya juu inapaswa kuwepo kila wakati bila mtumiaji kuchukua hatua yeyote.

Maswali ya kuuliza unapofanya uchunguzi huu ni;

- Ni hatua zipi data iliyokusanywa hupitia katika mifumo yako ya usindikaji?
- Je, wanaotumia mifumo yako wanahitajika kuchukua hatua gani wanapotumia ama kujumuishwa kwa mifumo yako ya usindikaji?
- Je, data inalindwa muda tu inapokusanywa?
- Je, wafanyikazi wanajua maana ya faragha na ulinzi wa data?
- Maswala ya ukiukaji wa faragha yanaripotwiwa na kutatuliwa vipi?
- Je, wateja wanajulishwa kuhusu maswala ya ukiukaji wa faragha?

**6. Uchambuzi wa Haki** – Shughuli za usindikaji wa data lazima zizingatie haki binafsi za wenye data husika, na ziepuke kukiuka haki zao na za familia zao. Haki hizi zinajumuisha haki zote za kibinadamu na pia haki maalum za data:

Haki hizi zimeoredheshwa kwenye DPA na ni;

Haki za Faragha	Maelezo
Haki ya kupata habari	Wateja wanapaswa kufahamishwa jinsi data zao zinatumiwa
Haki ya kuweza kufikia na kupata data binafsi	Wateja wanapaswa kuwa na uwezo wa kuangalia data zinazowahusu
Haki ya kupinga usindikaji	Wateja wana haki ya kupinga usindikaji wa sehemu ya au ujumla wa data yao. Shirika linapaswa kuwa na mipangilio inayorahisisha wateja kupinga usindikaji wowote
Haki ya kurekebisha data zisizo za kweli na za kupotosha	Shirika lazima liwe na mipangilio inayoweza wateja kuomba, kwa urahisi, data zisizo za kweli na za kupotosha kusahihishwa
Haki ya kufuta data zisizo za kweli na za kupotosha	Shirika vile vile lazima liwaruhusu wenye data kuomba, kwa urahisi, ufutaji wa data zao zisizo za kweli na za kupotosha

Maswali yafuatayo yanaweza kutumika katika uchambuzi wa haki;

- Je, unakusanya au unasindika data nyeti kama data kuhusu hali ya afya, kabila, imani, data ya kibaolojia, hali ya ndoa, jinsia, maelezo ya familia na kadhalika?
- Je, habari nyeti zinaweza kutambulika na kudhibitishwa kutoka kwa data uliyo nayo?
- Ni watu wangapi wanaweza athiriwa data uliyo nayo ikifichuliwa?
- Je, shirika lako limewahi kumbwa na matukio ya uvunjaji au utumizi mbaya wa data?
- Kuna matishio gani kwa data uliyo nayo?
- Je, ni hatua gani zimewekwa kulinda data uliyo nayo dhidi ya matishio?
- Ni hatua gani za kishirika zimewekwa kulinda data dhidi ya kufichuliwa?
- Haki za wenye data zinazingatiwa vipi katika shughuli zako za usindikaji wa data?
- Ni nani anayeamua jinsi ya kushughulikia maombi ya wateja kuhusu data zao? kuna mifumo?
- Ni haki gani zinaathiriwa katika shughuli zako za usindikaji wa data?

Hatua zifuatazo zinaweza kuchukuliwa baada ya kukamilisha uchambuzi wa haki;

- Uundaji au uboreshaji wa taratibu zinazo waruhusu wateja na wengine kufikia na kupata haki zao za data.
- Uundaji wa taratibu za binadamu kuingilia kati pale ambapo maombi ya mteja yanaedelezwa kiotomatiki
- Uundaji wa mifumo za usimamizi wa data; kwa mfano, kamati za kuzingatia maombi tata kutoka kwa wateja.

Baada ya chambuzi zilizopendekezwa katika hatua ya pili, ni muhimu kuchambua shughuli zote za usindikaji data zinazoenenezwa kwenye shirika lako kwa kijumla. Hii ni muhimu ilikutambua hatari au tishio zinazoweza ibuka. Pia, unaweza ashiria udhaifu wowote katika mifumo inayotumika kukusanya data, na pia kutambua pengo zilizopo katika mifumo ya kutathmini, na katika mifumo ya kuhifadhi data iliyokusanywa.

Mambo muhimu ya kuzingatia wakati wa uchambuzi wa kijumla ni;

- Mifumo na michakato – Mifumo yote inayokusanya data, jinsi data inapitishwa kati ya mfumo moja hadi nyingine, na wahusika wote katika shirika wanaopata na kutumia data iliyokusanywa kwa kazi mbalimbali.
- Data, kutoka mwanzo hadi mwisho – Hapa utazingatia mzunguko wa data tangu inapoingia kwenye shirika, jinsi inasindikwa, jinsi data hiyo inabadilika, ni lini data hiyo itastaafu, na jinsi data inafutwa.
- Udhaifu wa mifumo ya usindikaji – hapa utazingatia upeo wa athari ndani na nje ya shirika kukitukia kisa cha ukiukaji wa data katika shirika.
- Uslama wa mifumo
- Kiwango cha ujuzi na uendelezaji wa ulinzi wa data inayotambulika na washirika wa kampuni.
- Usimamizi wa data, inayojumuisha uhusiano na wasindikaji wengine wa data, na kushirikiana na wateja na umma.

Baada ya kukamilisha uchambuzi wa shughuli zote, hatua zifuatazo zinaweza fuata;

### **Ukizingatia data:**

- o Kushauriana na wateja ambao shirika lina data zao
- o Ukusanyaji wa data zaidi kuhakikisha usahihi wa data
- o Kuunganisha hifadhidata (data-sets)
- o Kufuta data zisizohitajika tena
- o Kufuta baadhi ya hifadhidata
- o Kurekebisha michakato ya shirika ili kuwa na usindikaji wenye ufanisi zaidi
- o Kurekebisha taratibu za ulinzi wa data ili kuimarisha ulinzi wa data binafsi
- o Kuunda upya mifumo ya usindikaji wa data kuzingatia faragha

### **Ukizingatia usimamizi wa data:**

- o Kupitia upya mikataba iliyopo na wasindikaji wengine wa data
- o Uundaji wa kamati za kulinda data
- o Uundaji wa misafa ya kupeana ripoti za ulinzi wa data
- o Kupanga upya kamati za usalama wa habari (information security committees) ili waendeleza shughuli za ulinzi wa data.
- o Kufanya ukaguzi wa mifumo (system audits)
- o Uteuzi wa afisa wa ulinzi wa data (data protection officer)
- o Kusimamia usimamizi data (data governance)
- o Kufunza wafany kazi wote kuhusu ulinzi wa data.
- o Kuandika mwongozo wa ulinzi wa data itakayotumika na shirika lako



## Hatua ya Nne

## Kutathmini tishio

Usindikaji wa data una uwezo wa kuhatarisha haki ya faragha, na kufichua data binafsi za wenye data husika. Kwa mfano, data inaweza kupotea au kuibiwa. Ili kutathmini kiwango cha matishio, unaweza zingatia hatua zifuatazo:

- tambua matishio mbalimbali
- Unda mfumo wa kuainisha matishio tofauti. Kwa mfano (tazama jedwali iliyo chini);
- Kuweka hatua za kupunguza hatari/tishio, kulingana na kiwango cha hatari/tishio

Uzito wa athari	Athari kubwa	Hatari ndogo	Hatari kubwa	Hatari kubwa
	Athari ya kati	Hatari ndogo	Hatari kiasi/ya kati	Hatari kubwa
	Athari ndogo	Hatari ndogo	Hatari ndogo	Hatari ndogo
	Kwa umbali	Uwezekano mzuri/ya kati	Uwezekano mkubwa	
	Uwezekano wa madhara/hatari/tishio			

Nukuu la Jedwali hili : ICO

## Hatua ya Tano

## Ripoti ya DPIA

Baada ya hatua hizi zote za kutathmini athari za ulinzi wa data, ripoti itaandikwa. Ripoti hii inapaswa kuidhinishwa na wasimamizi wa shirika husika. Baadhi ya yanayofaa kujumuishwa kwenye ripoti ya DPIA ni:

- a. Shughuli zote za usindikaji wa data;
- b. Uchambuzi wa kila shughuli na hatua zilizotumika kuendeleza shughuli hizo;
- c. Uchambuzi wa jumla wa shughuli zote za usindikaji katika shirika husika;
- d. Utambulishaji wa hatari/tishio; na
- e. Mapendekezo ya hatua shirika linafaa kuchukua ili kuzingatia sheria ya data na kupunguza hatari/tishio kwa wateja husika.

Matumizi na shughuli za usindikaji wa data katika mashirika mbalimbali lazima ya tathminiwe mara kwa mara; ili kuimarisha haki za faragha/usiri na ulinzi wa data ndani ya shirika, na pia kuimarisha haki za faragha kati ya shirika na wateja wanaohusika.

**Ufuatiliaji** - kufuatiliwa kwa shughuli za usindikaji wa data ili kutabiri matukio yanayoweza kuathiri haki za wateja husika.

**Ukadiriaji**-kuhakishakuwa hatua za ulinzi wa data zinatekelezwa kwa njia inayofaa, na kama hatua hizo zinafanya kazi zipoavyo.

Ufuatiliaji na ukadiriaji wa Tathmini ya Athari za Ulinzi wa Data

<b>Ufuatiliaji</b>	<b>Ukadiriaji</b>
<ul style="list-style-type: none"><li>- Fuatilia shughuli za usindikaji wa data</li><li>- Tambua matukio ya ulinzi wa data</li><li>- Tarajia matukio ya ulinzi wa data</li><li>- Hatimaye: Pendekeza mabadiliko kwa usimamizi ifaavyo</li></ul>	<ul style="list-style-type: none"><li>- Chunguza umuhimu wa mifumo ya ulinzi wa data katika shirika.</li><li>- Changanua kama hatua za ulinzi wa data zinatimiza malengo ya DPA</li><li>- Hatimaye: Mafunzo na mapendekezo ya Tathmini ya Athari za Ulinzi wa Data ya baadaye</li></ul>

## **Hitimisho**

Kwa muhtasari, DPIA ni shughuli ambayo shirika linapaswa kufanya ili kuelezea shughuli zake za usindikaji, kutathmini tishio/hatari zinazoweza ibuka dhidi ya haki na uhuru wa watu husika shughuli hizi zikitekelezwa, na kuweka hatua zinazofaa ili kupambana na au kupunguza hatari hizo. Tunatumahi kuwa maelezo haya yatakusaidia kufanya DPIA yako, na kukuongeza maarifa kuhusu Sheria ya DPA ya Kenya.

Pata rasilimali yote kwa lugha ya Kiingereza hapa: <https://cipit.strathmore.edu/wp-content/uploads/2021/05/Simplified-DPIA.pdf>



**Strathmore University**

---

*Centre for Intellectual Property and  
Information Technology Law*